**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**612** **URAIA**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2009**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org

TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Eleza uhusiano uliopo baina ya Azimio la Kazi na Muhtasari wa somo la Uraia.

2. Taja hoja nne zinazoeleza umuhimu wa kulinda rasilimali za umma kama mali ya taifa.

3. Eleza kwa kifupi hatua nne za kuzingatia wakati wa kufundisha dhana ya haki za binadamu ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kubaini haki hizo.

4. (a) Eleza maana ya uhuru wa habari.
   (b) Taja aina tatu za taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari kwa umma.

5. Onesha viashiria vinne vinavyoonesha kuwepo kwa ukiukwaji wa misingi ya utawala wa sheria.

6. Taja sifa nne za utendaji bora wa mwalimu wa somo la Uraia.

7. Kwa hoja nne, eleza umuhimu wa kutumia maswali ya hoja katika ufundishaji wa uraia.

8. Onesha faida zinazopatikana kutokana na kuwepo kwa mipango ya maendeleo ya jamii.

9. Toa mambo manne katika hotuba yako kama mgeni rasmi kwa wazazi wa shule ya msingi Mtakuja kubaini na kutambua umuhimu wa kufanya mitihani.

10. Toa hoja nne za umuhimu wa kuwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii

11. Eleza hoja tano zinazoonyesha mchango wa bunge katika kuimarisha utawala wa kidemokrasia.

12. Kwa kutumia hoja sita, fafanua athali za kutokua na usawa wa kijinsia katika ngazi ya familia na jamii.

13. Fafanua changamoto tano za kiuchumi zinazoweza kuikabili nchi inayoendelea kama Tanzania

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii

14. Onesha mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa somo la Uraia kwa matumizi ya darasani.

15. Fafanua hatua sita muhimu katika kutengeneza zana bora za kufundishia somo la Uraia kwa kutumia vifaa vinavyopatikana mazingira ya karibu.

16. Eleza kwa hoja sita umuhimu wa kufanya maandalizi ya Azimio la kazi katika somo la Uraia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org